



# PROGRAMU YA MWITIKIO YA NOVO NORDISK

## TAARIFA YA PROGRAMU

Programu ya Mwitikio ya Novo Nordisk ([www.nnrp.ca](http://www.nnrp.ca)) ni ya wahamiaji wapya na wakimbizi nchini Kanada ambao hawana njia ya kupata bima ya dawa na hawana fedha za kununua insulini za Novo Nordisk na sindano zake.

## MAELEZO YA PROGRAMU

Mpango wa Mwitikio wa Novo Nordisk hutoa insulini na sindano teuzi za Novo Nordisk kwa hadi siku 120 kuanzia tarehe ambayo kadi ya manufaa ya Mpango wa Mwitikio ya Novo Nordisk ya mgonjwa itaanza kutumika.

Programu hii inanuiwa kutoa msaada **wa muda** wakati wagonjwa wanapata bima ya kibinafsi / bima ya ziada ya dawa au kutuma maombi ya programu ya dawa za umma.

Kama bima ya kibinafsi/bima ya ziada ya dawa imepatikana ndani ya siku 120 za kuanza kutumia Programu ya Mwitikio ya Novo Nordisk, manufaa ya Programu ya Mwitikio ya Novo Nordisk baadaye huachishwa.

## KADI YA MANUFAA YA PROGRAMU

Kadi za Manufaa za Programu ya Mwitikio ya Novo Nordisk hutolewa kwa wagonjwa na wataalamu wao wa afya.

## MSAADA KWA VIFAA VYA UTOAJI WA INSULINI

- [FlexTouch® Video ya Maonyesho ya Kudunga Sindano \(Kiingereza\)](#)
- [NovoPen® 4 Video ya Maonyesho ya Kudunga Sindano \(Kiingereza\)](#)
- [NovoPen® Echo® Video ya Maonyesho ya Kudunga Sindano \(Kiingereza\)](#)

## UNAYO MASWALI ZAIDI?

Kwa taarifa zaidi kuhusu Programu ya Mwitikio ya Novo Nordisk, wasiliana na Huduma ya Wateja ya Novo Nordisk katika 1-800-465-4334.



# PROGRAMU YA MWITIKIO YA NOVO NORDISK

## MAJUMUISHO YA BIDHAA

<b>Tresiba®</b>	2467860 - Tresiba® Penfill® 2467879 - Tresiba® U-100 FlexTouch® 2467887 - Tresiba® U-200 FlexTouch®
<b>NovoRapid®</b>	2377209 - NovoRapid® FlexTouch® 2244353 - NovoRapid® Penfill® 2245397 - NovoRapid® Vial
<b>Levemir®</b>	2412829 - Levemir® FlexTouch® 2271842 - Levemir® Penfill®
<b>NovoMix®</b>	2265435 - NovoMix® 30 Penfill®
<b>Novolin® ge 30/70</b>	2025248 - Novolin® ge 30/70 Penfill® 2024217 - Novolin® ge 30/70 Vial
<b>Novolin® ge NPH</b>	2024268 - Novolin® ge NPH Penfill® 2024225 - Novolin® ge NPH Vial
<b>Novolin® ge Toronto</b>	2024284 - Novolin® ge Toronto Penfill® 2024233 - Novolin® ge Toronto Vial
<b>Sindano</b>	NovoFine® 32G Tip etw x 6 mm

## NOVOPEN® UPATIKANAJI

**NovoPen® 4** vifaa vinapatikana kwenye duka la dawa bila gharama yoyote kwa wagonjwa.

**NovoPen® Echo®** vifaa vinaweza kupatikana, kwa kuomba, katika ofisi ya Mtaalamu wa Huduma ya Afya au katika Kituo cha Elimu ya Kisukari cha mtaani. Aidha, wanafamasi wanaweza kuomba vifaa vya NovoPen® Echo® kwa viwango vichache kwa kuwasiliana na Huduma ya Wateja ya Novo Nordisk katika: 1-800-465-4334.

Bidhaa zilizojumlishwa kwenye programu hii ziko kwa hiari ya Novo Nordisk Canada Inc. na zinaweza kubadilishwa bila arifa ya mapema.



# PROGRAMU YA MWITIKIO YA NOVO NORDISK

## MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA

### → Je, kadi ya manufaa inaweza kutumika kwa zaidi ya dawa moja ya Novo Nordisk?

Ndiyo! Kadi ya manufaa ya Programu ya Mwitikio ya Novo Nordisk inaweza kurudishiwa thamani yake kwa tiba moja ambayo imelipiwa au mchanganyiko wowote wa insulini uliolipiwa wa Novo Nordisk.

### → Je, kadi ya manufaa ya Programu ya Mwitikio ya Novo Nordisk inaweza kutumika kwa zaidi ya mara moja?

Ndiyo! Manufaa hayohayo, kadi ya manufaa ya Programu ya Mwitikio ya Novo Nordisk inaweza kutumika kujaza tena insulini hadi siku 120. Pia, Programu ya Mwitikio ya Novo Nordisk hutoa sanduku 1 ya sindano kwa kila kadi ya manufaa iliyorudishwa (hadi upeo wa masanduku 4).

### → Je kadi ya manufaa ya Programu ya Mwitikio ya Novo Nordisk ina muda wa kuisha?

Programu ya Mwitikio ya Novo Nordisk iliundwa ili kutoa utulivu wa muda wa watu wapya nchini Kanada. Kadi ya manufaa ya programu hukakikisha ufikivu wa insulini ya Novo Nordisk teuzi na sindano hadi siku 120. Ndani ya siku hizo 120, wapokeaji wa programu huhimizwa kununua bima ya dawa ya kibinafsi / bima ya ziada ya dawa au kutuma ombi ya programu mbalimbali za dawa za serikali za mkoa na kimaeneo.

Kama bima ya kibinafsi/bima ya ziada ya dawa imepatikana ndani ya siku 120 za kuanza kutumia Programu ya Mwitikio ya Novo Nordisk, manufaa ya Programu ya Mwitikio ya Novo Nordisk baadaye huachishwa.

### → Je, kuna gharama au malipo ya insulini ya Novo Nordisk iliyojumuishwa?

La. Programu ya Mwitikio ya Novo Nordisk hulipia gharama ya dawa na sindano zilizotengenezwa na Novo Nordisk pamoja na viwango vya alama za tasnia na ada za usambazaji.



# **PROGRAMU YA MWITIKIO**

---

## **YA NOVO NORDISK**

→ **Sindano zimejumuishwa kwenye Programu ya Mwitikio ya Novo Nordisk?**

Sindano teuzi ndizo zimejumuishwa katika programu hii. Programu ya Mwitikio ya Novo Nordisk hutoa sanduku 1 ya sindano kwa kila kadi ya manufaa iliyorudishwa (hadi upeo wa masanduku 4).

→ **Je, ni wapi ninaweza kupata maelezo zaidi kuhusu programu mbalimbali za manufaa za dawa za umma za mkoa na kimaeneo?**

Tembelea ukurasa wa [Programu za dawa za Umma za Mkoa na Kimaeneo](#) ulio kwenye tovuti ya Serikali ya Kanada kwa taarifa zaidi.